# KUFAA KWA NADHARIA YA UCHANGANUZI VIJENZI KATIKA UCHAMBUZI WA HIPONIMIA

*Benard Odoyo Okal, Florence Indede*
na
*Ernest Sangai Mohochi*

**Ikisiri**

*Hiponimia ni mojawapo ya mahusiano ya kifahiwa inayoashiria uhusiano ambapo leksimu ya jumla inajumuisha kimaana leksimu mahususi. Uhusiano wa leksimu kihiponimia ulidhukuriwa kuwa unafanana katika lugha anuwai ulimwenguni na aghalabu unahusisha leksimu nomino pekee. Hata hivyo, tafiti za hivi punde zinadhihirisha kuwa hiponimia huonekana pia miongoni mwa vivumishi, vielezi na vitenzi na huweza kutofautiana kimuundo na kimtindo kutoka lugha moja hadi nyingine kwa sababu ya tofauti za kitamaduni. Wataalamu anuwai wamekuwa na mapendekezo kadha kuhusu nadharia ifaayo ya kuainisha leksimu za lugha kihiponimia. Wengine wanaelekea kupendelea matumizi ya nadharia ya Kiini Maana (Core Meanings Theory) na Nadharia ya Sampuli Kifani (Prototype Theory). Hata hivyo inadhihirika kuwa nadharia ya Uchanganuzi Vijenzi (Componential Analysis) inafaa zaidi katika uchanganuzi wa hiponimia ya leksimu nomino, vitenzi, vivumishi na vielezi. Makala haya yanaangazia kufaa kwa nadharia hii katika uhakiki wa hiponimia ikilinganishwa na nadharia Kiini Maana na Sampuli Kifani.*

## 1.0 Utangulizi

Kazi hii inapambanua matumizi ya nadharia ya Uchanganuzi Vijenzi katika uhakiki wa hiponimia. Inaangazia maana ya nadharia ya Uchanganuzi Vijenzi, chimbuko lake, maendeleo yake, ufafanuzi wa mielekeo ya sifa za leksimu katika hiponimia, taratibu zake, natija na udhaifu wake. Kuna vilevile uchanganuzi wa kufaa kwa nadharia ya Uchanganuzi Vijenzi ikilinganishwa na nadharia nyingine kama vile Nadharia ya Kiini Maana (*Core Meanings Theory*) na Nadharia ya Sampuli Kifani (*Prototype Theory*).

## 1.1 Nadharia ya Uchanganuzi Vijenzi

Nadharia ya Uchanganuzi Vijenzi inamaanisha kuwa leksimu jumuishi (hipanimu) ya lugha ina maana yake na maana hiyo husika hujengwa kutokana na maana za leksimu nyingine mahususi (hiponimu) ambazo zinaonyesha sifa kadhaa bainifu (Asher, 1994). Nadharia hii inahusisha matumizi ya seti ya sifa bainifu za kisemantiki za kuonyesha maana za leksimu mahususi ili kuzibainisha katika uwanda wake maalum (Jensen, 2008; Saeed, 2009). Aghalabu sifa hizi bainifu

huwa na mipaka maalum huku jozi ya sifa zenyewe zikioneshwa kutokana na matumizi ya alama kama vile [+, -] ambapo [+] huonesha kuwepo kwa sifa na [-] hutumiwa kuonyesha kutokuwepo kwa sifa fulani inayorejelewa (Jensen, 2008; Saeed, 2009). Mtindo kama huu ulirejelewa kama wa kisarufi zalishi ambapo sifa bainifu kadhaa huzalishwa ili kusaidia katika kutofautisha leksimu moja na nyingine katika uwanda mmoja kileksika na kisemantiki. Kama vile leksimu jumuishi *kijana* hujumuisha kimaana leksimu mahususi hasa [*msichana* na *mvulana*]. Hata hivyo, leksimu *msichana* ina sifa bainifu kama vile [+kike, -kiume] huku leksimu *mvulana* ikiwa na sifa bainifu maalum kama vile [+kiume, -kike]. Hata hivyo, leksimu zote zina sifa inayofanana ya [+kijana].

**1.2 Chimbuko na Maendeleo ya Nadharia ya Uchanganuzi Vijenzi**

Nadharia ya Uchanganuzi Vijenzi ilichipuka kutokana na maendeleo ya Nadharia ya Uwanda Kisemantiki (Semantic Field Theory) iliyoasisiwa na Jost Trier katika miaka ya 1934 (Bussmann, 1996). Kwa mujibu wa Nadharia ya Uwanda Kisemantiki, leksimu za lugha huwa na seti maalum inayojumuisha leksimu mahususi zinazohusiana kutokana na mtazamo wa sifa husika za viashiriwa na maana (Bussmann, 1996). Madhumuni yake ni kuonyesha hali kwamba maana ya leksimu haufai kufanywa tu kwa kurejelea leksimu hiyo moja pekee bali kwa kuhusisha na leksimu nyingine (Crystal, 1992). Hivyo basi, nadharia ya Uwanda Kisemantiki ni njia mojawapo ya kuweka mtindo maalumu katika maelezo ya misamiati ili kuipanga katika njia mbalimbali (Crystal, 1987). Nadharia ya Uwanda Kisemantiki wakati mwingine hurejelewa pia kama nadharia ya Uwanda Kileksika (Crystal, 1992) ulioangaziwa katika miaka ya 1963 na kina Heinz Werner na Benard Kaplan katika kazi yao iliyoitwa *'Symbol Formation'* (Miller, 1991). Uwanda Kisemantiki hurejelea maana ya kundi la leksimu husika na Uwanda Kileksika hurejelea jina la kundi lenyewe. Mathalani, *mfugo* kama uwanda kileksika unajumuisha hiponimu kama vile [*kondoo, mbuzi, ng'ombe, punda*] na unahusisha uwanda kisemantiki wenye maana ya wanyama wanaofugwa.

Uwanda kileksika unaweza kuwa mpana kutokana na jinsi leksimu zinavyohusiana na idadi ya leksimu husika. Mabadiliko katika maana ya leksimu mahususi katika uwanda mmoja kileksika huleta vilevile mabadiliko katika jina la uwanda kisemantiki (Krifka, 2001). Kwa mfano, uwanda kileksika unaoitwa *nguo* hujumuisha leksimu mahususi kama vile [*fulana, kaptura, rinda, shati, suruali*]. Hata hivyo, iwapo leksimu *kiatu* itaingizwa katika kundi hili basi bila shaka maana ya leksimu ya jumla itabadilika na hatimaye kurejelewa kama *vazi*. Mfano mwingine unaonekana pia miongoni mwa leksimu zinazohusisha *sehemu za mwili* zinazojumuisha hiponimu kama vile [*kichwa, kiwiliwili, miguu, mikono, shingo*].

Kundi hili likiongezewa leksimu mahususi inayotofautiana kifahiwa kama vile *mkongojo* basi maana na jina la jumla la sehemu hizi za mwili hupotea.

Mtindo wa kupanga Leksimu katika mawanda ulitumiwa na wanaanthropolojia kama njia moja maalumu ya kulinganisha msamiati kutoka tamaduni mbalimbali. Baadaye ukaboreshwa zaidi na wanasemantiki kama fomula maalumu ya kuchanganua maana za leksimu husika. Fomula inayozungumziwa huundwa kwa kutumia vipashio vidogo vya sifa bainifu kama vile [utu zima, mtoto, kike au kiume] na alama [+, -] za kuonyesha vipashio hivyo vidogo hutumiwa katika matriki ili kuweza kuzitofautisha maana za leksimu husika (Crystal, 1987).

Nadharia ya Uwanda Kisemantiki ilitumiwa katika nyanja mbalimbali kama vile kuonyesha ubia katika *upishi* (Lehrer, 1974). Uchunguzi wa ulinganifu wa leksimu zinazojumuishwa katika *upishi* ulifanywa miongoni mwa lugha za Kifaransa, Kijerumani, Kiajemi, Kipolandi, Kijapani, Kichina, Kijakaliteki (Jacaltec), Ki-Amharaki, Kinavaho na pia Kiyoruba (Lehrer, 1974). Uwanda kisemantiki unaoitwa *upishi* unatokana na kitenzi *pika* na hujumuisha aina mbalimbali za upishi kama vile *tia mvuke, chemsha, kaanga, banika* (broil), *choma* (roast), *oka* (bake) (Lehrer, 1974). Kwa upande mwingine, *chemsha* hujumuisha *chemsha kwa nguvu* (boil), *chemsha polepole bila kiputo* (simmer). C*hemsha bila kiputo* hujumuisha *vukiza yai* (poach), *chemsha polepole majini* (stew), *pika kwa mvuke* (braise). *Kaanga* (fry) hujumuisha *kaanga upesi kwa mafuta kidogo* (sauté), *kaanga kwa mafuta mengi* (deep fry) huku *banika* (broil) ikijumuisha *choma* (grill) na *ikari* (barbecue).

Nadharia ya Uwanda Kisemantiki ilitumiwa pia na mwanasaikolojia Mjerumani aitwaye Karl Buhler alipoandika *'Language Theory: The Representational Function of Language'* ya miaka ya 1934 (Miller, 1991). Buhler aliainisha mawanda ya leksimu katika 'uwanda ashiria' (pointing field) unaosaidia ufahamu wa maana za maneno kama vile *wewe, hapa* na *sasa* yanayodokeza maana kwa mujibu wa mahali na muktadha. Vilevile alichanganua 'uwanda kisintaksia' (syntactic field) unaoonyesha kuwa leksimu mahususi hazitoi maana kamilifu zikiwa pekee bali hupata maana zikihusiana na nyingine katika uhusiano mlalo.

Kutokana na maendeleo ya Nadharia ya Uwanda Kisemantiki na Uwanda Kileksika, Nadharia ya Uchanganuzi Vijenzi ikachipuka. Hivyo basi, Nadharia ya Uchanganuzi Vijenzi inaweza kudhukuriwa kama mbinu mojawapo ya kuelezea uwanda kisemantiki (Koulikova, 2006). Baada ya kuchipuka kwake, kulitokea mielekeo mbalimbali ya wataalamu wa Ulaya na Marekani kuhusiana na nadharia hii (Koulikova, 2006). Mwelekeo wa awali kutoka Ulaya ulionekana katika kazi ya Hjemslev ya 1943 na pia miaka ya 1960 hasa kutokana na juhudi za akina Pottier,

Coseriu na Greimas (Asher, 1994; Koulikova, 2006). Katika nyakati hizo za wataalamu hawa, Nadharia ya Uchanganuzi Vijenzi ilitumiwa kuonyesha kuwa elementi katika uwanda mmoja wa kileksika na kisemantiki hutofautishwa kutokana na ukinzani wake kiuamilifu (Asher, 1994). Ukinzani kiuamilifu baina ya leksimu katika uwanda mmoja unadhihirika kutokana na mwelekeo wa uchunguzi kiuana, kizazi, kwa mujibu wa rangi na hata umbo na kila uchunguzi ulifanywa kwa kutumia sifa bainifu. Sifa hizi bainifu zinaeleza jinsi leksimu katika seti maalum zinavyohusiana na nyingine na jinsi zinavyotofautiana licha ya kuwa katika uwanda maalumu kileksika na kisemantiki (Wardhaugh, 1977; Kreidler, 2002).

Licha ya kwamba Nadharia ya Uchanganuzi Vijenzi iliibuliwa kuonyesha mfumo maalum wa uhusiano wa leksimu katika uwanda kileksika na kisemantiki. Vilevile iliweza kuhusishwa na wanaleksikografia ambapo leksimu za lugha zinafasiliwa kwa kuchambuliwa katika viambajengo vidogo. Kama vile fasili ya leksimu *kondoo dume* (ram) huweza kutolewa kwa kutumia [*kondoo wa kiume*] ili kuitofautisha na leksimu nyingine zinazotumiwa katika uwanda kileksika na kisemantiki unaoitwa *kondoo* (Asher, 1994). Hivyo basi, sifa bainifu za *kondoo dume* ni [+kiumbe hai, +kondoo, +wa kiume] ili kuitofautisha na *kondoo* wengine.

Nadharia ya Uchanganuzi Vijenzi ilichota mtindo wake pia kutokana na taaluma ya fonolojia ya kutambua fonimu ambapo alama [+, -] zilitumiwa ili kutofautisha sifa za fonimu moja na nyingine (Asher, 1994). Mbinu za kutambua sifa za fonimu zilidokezwa na wataalamu wa skuli ya Prague waliofasili sauti kwa kurejelea kuwepo au kutokuwepo kwa sifa zake bainifu (Jackson, 1996). Shule ya mawazo ya Prague walikuwa wakishughulikia masuala ya umuundo na uzalishaji katika taaluma ya fonolojia kwa kutumia sifa kama vile [+, -] ili kubainisha fonimu husika (Krifka, 2001). Mmoja wa wanaskuli wa Prague alikuwa Trubetzkoy aliyeeleza kuwa fonimu hufasiliwa kwa kutumia kigezo cha sifa za kisaikolojia au sifa za kifonetiki na pia sifa za kiuamilifu katika mfumo wa fonolojia ya lugha maalum (Mgullu, 1999).

Sifa za kifonetiki husaidia kutofautisha fonimu ambazo zinapatikana katika kundi fulani. Kwa kutumia alama [+, -] tunaweza kubainisha sifa za fonimu vokali za nyuma /u, o/ na za mbele /i, e/ kama vile: /u/ ina sifa [+irabu, +nyuma, +juu, +mviringo] na /o/ ina sifa [+irabu, +nyuma, +nusujuu, +mviringo] huku /i/ ikiwa na sifa [+irabu, +mbele, +juu, -mviringo] na /e/ ina sifa /+irabu, +mbele, +nusujuu, -mviringo] (Mgullu,1999: 32). Sifa zinazoonyesha tofauti baina ya irabu hizi ni kuwa/o, u/ zina sifa bainifu [+mviringo] huku /i, e/ zikiwa na sifa bainifu [-mviringo]. Sifa hizi za kifonetiki ndizo zinazochangia tofauti za maana katika fonimu na maana ya leksimu husika. Mathalani, tukiwa na leksimu zenye fonimu

mbili /e, u/ katika leksimu kama vile ***peta*** na ***puta***, basi kutokana na sifa bainifu baina ya /e/ kuwa [+nusujuu, -mviringo] na /u/ kuwa na sifa [+juu, +mviringo], leksimu hizi vilevile zinatofautiana kimaana.

Kwa kutumia leksimu zenye mlinganuo finyu (leksimu zenye idadi sawa za fonimu hata hivyo fonimu moja katika kila leksimu kuwa na sura tofauti) (Mgullu, 1999), mtindo wa nitoe nikutoe unaweza kutumiwa ili kudhihirisha tofauti zake kimaana kama tunavyoonyesha katika jedwali lifuatalo:

**Jedwali 1: Matumizi ya Mtindo wa Nitoe Nikutoe baina ya Leksimu**

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| *peta* | p̸ | e | t̸ | a̸ | =/e/ |
| *puta* | p̸ | u | t̸ | a̸ | =/u/ |

Baada ya kutumia mtindo wa nitoe nikutoe dhidi ya fonimu /p, t, a/, fonimu mbili zenye maumbo tofauti /e, u/ zinasalia. Hivyo basi, jinsi fonimu hizi mbili za /e, u/ zinavyokataa kutoana kwa kutumia mtindo wa nitoe nikutoe ndivyo vile zinavyoleta tofauti kimaana baina ya leksimu hizi mbili. Kama vile ***peta*** inamaanisha 'rusharusha nafaka katika kitunga au ungo ili kuondoa makapi na takataka' (TUKI, 2004:333) na ***puta*** inamaanisha 'piga nafaka k.v. mtama na mpunga ili kuutoa kwenye mashuke yake' (TUKI, 2004: 343).

Baadaye wataalamu wengine walianza kutumia nadharia ya Uchanganuzi Vijenzi katika semantiki (Krifka, 2001) kama vile Wamarekani Goodenough (1956) na Lounsbury (1963) walioshughulikia mahusiano ya watu kitabia na kiukoo. Nadharia hii iliendelezwa vilevile na Hjemslev (1970) na Katz na Fodor (1963, 1981) ambaye tumetumia mwelekeo wake. Vilevile nadharia hii imetumiwa katika fafanuzi mbalimbali za kazi za wataalamu kama vile Mathews (1997), Asher (1994) na Prinsloo na wenzake. (2000). Hjemslev (1970) alishughulikia 'glosematiki' (glossematics) inayotokana na neno 'glosemi' (glosemes) lenye maana ya kipashio kidogo zaidi cha lugha. Alichanganua vipashio vidogo vya lugha vinavyowekwa pamoja katika kategoria kuu na hatimaye kusaidia kubainisha kati ya kipashio cha jumla na mahususi pamoja na mahusiano yake.

Nadharia ya Uchanganuzi Vijenzi ilikuwa na nguvu kimatumizi kutokana na kazi ya Katz na Fodor (1963). Kimiliki kikuu cha nadharia hii ni kuhusisha seti ya sifa bainifu za kisemantiki za leksimu mahususi ili kuzibainisha katika uwanda maalum (Katz & Fodor, 1963, 1981). Hapo awali sifa hizi bainifu ziliwahi kupendekezwa katika mwelekeo wa kiurasimi wa Aristotle ili kuweka pamoja

leksimu zinazohusiana (Cruse, 2011). Nadharia ya Uchanganuzi Vijenzi ingali maarufu katika uchanganuzi wa leksimu katika mawanda kileksika (Katz, 2004).

**1.3 Mielekeo ya Sifa za Leksimu**

Kuna mielekeo miwili mikuu inayoweza kuzingatiwa kuonyesha sifa za leksimu tunapotumia nadharia ya Uchanganuzi Vijenzi katika hiponimia kama vile mwelekeo wa kiisimu na wa kisayansi. Sifa za leksimu kiisimu hutegemea vigezo vya kifahiwa au kimaana, kawaida na kiuamilifu, na kwa ujumla huzingatia ujuzi wa mtu kuhusu lugha yake kama vile [+ kawaida, +hisivu, +mguso, +utu, +hesabika]. Sifa hizi bainifu zinatumiwa kuonyesha kwamba kila leksimu ina idadi mahususi ya sifa zake ambazo aghalabu zinaonekana zikiathiri mazingira ya kisintaksia hasa tunapoangazia kategoria ya leksimu nomino kama vile [+- kawaida, +- hesabika, +- hisivu, +- utu, +- mguso] (Munyua, 1999). Tunaweza kutumia sifa hizi bainifu za kiisimu kuchanganua leksimu kama vile *mvulana* ina [+nomino, +kawaida, +hesabika, +utu, +kiume, -kike, +mguso, +kijana] na *msichana* ina [+nomino, +kawaida, +hesabika, +utu, +kike, -kiume, +mguso, +kijana]. Sifa zinazotofautisha leksimu hizi mbili ni kwamba *mvulana* ina sifa [+kiume, -kike] ilhali *msichana* ina sifa [+kike, -kiume].

Inabainika kuwa sifa za leksimu zinazohusiana kihiponimia zinazotumiwa pamoja na alama hizi za [+, -] aghalabu hazifanani (Lipka, 1986). Hii inamaanisha kuwa zinategemea uteuzi wa mchanganuzi mwenyewe. Mathalani, sifa ya kubainisha maana kama vile [+binadamu, -binadamu] inaweza kutumiwa kubainisha watu na wanyama kama vile *msichana* ina sifa [+binadamu] na *mwana farasijike* (filly) ina sifa [-binadamu]. Sifa hii inafaa hasa katika uchanganuzi wa hiponimia katika nomino zenye uhai. Sifa nyingine ya kiisimu hutumiwa kuonyesha maana kimatilaba kama vile [+kizamani/kikale, -kizamani/kikale] kama tunavyoona katika leksimu *farasi bora* (steed) yenye sifa [+kizamani] na *farasi* ya kawaida yenye sifa [-kizamani]. Kuna pia sifa ya kuonyesha uhusiano kama vile [+-mzazi wa] kama inavyoonekana baina ya *mzazi* na *mwana*.

Kunaonekana pia sifa ya kuhamishwa maana kama katika vitu viowevu au majimaji kama vile [+kiowevu, -kiowevu] kama tunavyoona katika leksimu zinazorejelea vitu majimaji vya kunywewa. Sifa hii inaweza kutumika katika uchanganuzi wa hiponimia za vyakula ambapo pana vyakula viowevu na vigumu kama vile *mchuzi* ina [+chakula, +majimaji/kiowevu, -kigumu] na *biskuti* ina [+chakula, -kiowevu, +kigumu]. Aidha, tunaweza kuwa na sifa ya kurejelea kionyeshi kibainishi kama vile [+karibu, -karibu] kama tunavyoona baina ya vielezi wakati kama vile *sasa* [+karibu] na *wakati uliopita* [-karibu]. Kuna pia sifa ya kuangazia urejeshi wa kifaa kitumizi kama vile [+kiboko, -kiboko] kama katika *piga* (beat) [+kwa kiboko] na *kuashiria kwa kudukua/kugusa na kiwiko* (nudge)

hasa unapotaka huduma [-kwa kiboko]. Hivyo basi, kuna matumizi anuwai ya sifa bainifu ya kuonyesha tofauti baina ya leksimu moja na nyingine.

Uainishaji wa kiisimu wa sifa za leksimu unampa mtafiti uhuru wa kuongezea sifa bainifu nyingine jinsi anavyotaka hadi apate tofauti za leksimu husika ambazo hujumuishwa katika hipanimu maalum. Mathalani, hiponimu [*kabati, kigoda, kiti, kitanda, meza*] zina sifa za kiuamilifu kwa hivyo huainishika katika hipanimu *fanicha*. Uainishaji wa kiisimu wa sifa za leksimu hutusaidia katika mlinganisho wa hiponimia za lugha mbili tofauti kama tunavyoona baina ya Kiswahili na Kiluo. Mathalani, leksimu hipanimu *mzazi* (*janyuol*) inajumuisha kiisimu hiponimu [*baba* (wuoro) na *mama* (miyo)] kwa sababu zote zina sifa zinazofanana za [+mnyama, +binadamu, +utu zima]. Hata hivyo zina sifa bainifu kama vile *baba* ina sifa bainifu [+kiume, -kike] na leksimu *mama* ina sifa bainifu [+kike, -kiume]. Kisawe cha *baba* katika Kiluo ni *wuon* au *wuoro* huku kisawe cha mama ni *min* au *miyo*. Hali hii ya kuwa na jinsi mbili za kurejelea visawe hivi hutokea kwa sababu ya msingi wazi na umilikaji. *Wuoro* na *miyo* hurejelewa kwa kutumia msingi wazi (bare form) huku *wuon* na *min* huonyesha umilikaji (possessed form) (Tucker, 1994; Cable, 2009).

Kwa ujumla, sifa za leksimu zinazochunguzwa kiisimu zinaweza kuanishwa katika aina mbili kuu za: kawaida zinazolingana miongoni mwa leksimu zote katika uwanda mmoja na pia sifa bainifu zinazoonyesha tofauti baina ya leksimu husika katika uwanda maalum (Nida, 1975). Tunapochunguza sifa hizi bainifu za leksimu husika, tunaweza kutambua kuwa vijenzi vyote vya hipanimu haviwezi kugawika zaidi kimaana kuliko jinsi vinavyoonekana (Aitchison, 2003). Tukichukua kwa mfano sifa tatu za [binadamu, utu zima, kiume] za kulinganishwa katika uchanagnuzi wa sifa bainifu za *mwanamume, mwanamke, mvulana* na *msichana*, basi tutapata kuwa zote zina sifa zinazolingana za [+binadamu]. Hata hivyo zinatofautiana kwa sababu *mwanamume* ina sifa [+kiume], *mwanamke* [-kiume], *mvulana* [-utu zima, +kiume] na *msichana* [-utu zima, -kiume] (Leech, 1976) ambazo haziwezi kugawika zaidi. Mara nyingi sifa bainifu za leksimu huangaziwa kwa kutumia majedwali ili ziweze kutambulika haraka kwa wasomaji. Hivyo basi, leksimu hizi za *mwanamume, mwanamke, mvulana* na *msichana* zina sifa bainifu zifuatazo kama zinavyoonyeshwa katika jedwali lifuatalo:

**Jedwali 2: Matumizi ya Mtindo wa Nitoe Nikutoe baina ya Leksimu**

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| *peta* | p✓ | e | t✓ | a✓ | =/e/ |
| *puta* | p✓ | u | t✓ | a✓ | =/u/ |

Licha ya kuwa sifa hizi bainifu za leksimu kama zinavyoelezwa na Lipka (1986) zinaelekea kuangaziwa kiisimu, kwa upande mwingine kuna sifa bainifu zinazoweza vilevile kuelezwa kwa njia mchanganyiko za kisayansi na kiisimu (Asher, 1994). Mwelekeo wa kisayansi aghalabu hurejelea vigezo vya sifa asilia za kibiolojia ambazo hazionekani kwenye leksimu zenyewe bali kwa kuangazia sifa halisia za virejelewa katika mazingira maalum (Fromkin, Rodman na Hyams, 2007). Kama vile *mamalia* huweza kuchanganuliwa kibiolojia kwa kutumia sifa: [+uti wa mgongo, +ufunikaji mwili, +ukakawana maungo ya mwili, +utanafusi au upumuaji, +mzunguko/mwenezo wa damu, +utoaji taka mwilini, +uundaji na michomozo ya kemikali za mwili, +mishipa ya fahamu, +uzazi, +mmeng'enyo]. Sifa hizi za kibiolojia pamoja na sifa ya kunyonyesha watoto husawiri pia hiponimu kama vile [*binadamu, nyani, kima* na *sokwe*] ambazo hujumuishwa kisayansi katika hipanimu *mamalia*.

**1.4 Taratibu za Nadharia ya Uchanganuzi Vijenzi**

Nida (1975) anaeleza kuwa kuna taratibu sita muhimu zinazofuatwa tunapotumia Nadharia ya Uchanganuzi Vijenzi katika uchanganuzi wa hiponimia kama vile: kwanza, kufanya uteuzi wa awali kuhusu maana za hiponimu zinazoweza kujumuishwa katika hipanimu. Kama vile hipanimu *binadamu* hujumuisha hiponimu kadha zenye sifa maalum zinazofanana na zinazoonyesha uhusiano kwa mujibu wa damu au ndoa za viashiriwa na pia kiuamilifu. Hivyo basi, sifa maalum za *binadamu* huonekana katika utoaji wa maana za leksimu kama vile *baba, mama, mtoto wa kiume, mtoto wa kike, ndugu wa kiume* na *wa kike, mjomba, shangazi, binamu* na kadhalika.

Pili, kuorodhesha hiponimu zinazolingana kwa kiwango fulani katika maana ya hipanimu husika. Utaratibu huu unaweza kutumiwa katika tafiti za kileksikografia huku maana ya hipanimu ikiangaziwa katika kamusi kisha hiponimu zake huorodheshwa kialfabeti ili kurahisisha uchanganuzi hivyo basi uteuzi wa hiponimu hufanywa kwa kuzipanga kialfabeti kutoka A hadi Z ili kurahisisha uchanganuzi. Tatu, kubainisha zile hiponimu husika ambazo zina maana zinazofungamana kwa kurejelea sifa kadha zinazoangaziwa kwa kutumia alama kama vile [+, -]. Nne, kubainisha sifa za kimsingi zinazolingana na viashiriwa husika kama vile [binadamu, kiume, uana, kizazi] kama tunavyoona katika *baba* [+binadamu, +kiume] na *mama* [+binadamu, -kiume]. Tafiti nyingi za kileksikografia hutumia sifa za kiisimu ambapo mtafiti anakubaliwa kukadiria na kutathmini kufaa kwa sifa husika za kutumiwa. Tano, kupitia tena data iliyokusanywa kwa mujibu wa utaratibu wa kwanza ili kuweza kuonyesha ipasavyo sifa husika na vilevile kuzirekebisha ipasavyo. Sita, kufasili sifa za hiponimu husika kwa kutumia mfumo maalum kwa kutumia kielelezo tungo au majedwali.

Baada ya kutambua hipanimu ya hiponimu maalum, mtafiti anapaswa pia kuzingatia taratibu nyingine za kiisimu kama anavyoeleza (Nida, 1975) kama vile kwanza, kupatia kila hipanimu jina lake maalum kama vile *mnyama* na kutoa maelezo mafupi kama vile *mnyama* 'kiumbe hai ambacho kwa kawaida huwa na miguu minne k.v. ng'ombe, sungura n.k.' (Longhorn, 2011: 336]. Pili, kutoa fasili ifaayo ya kidahizo hiponimu kama vile *simba* 'mnyama mkubwa wa porini wa jamii ya paka mwenye manyoya ya rangi ya majani makavu na ambaye hula nyama' (TUKI, 2004:375). Tatu, kuainisha kimakundi hiponimu zenye sifa zinazofanana, kutenganisha sifa bainifu na kueleza sababu maalum za kuweka hiponimu katika uwanda huo husika.

**1.5 Natija za Nadharia ya Uchanganuzi Vijenzi**

Nadharia ya Uchanganuzi Vijenzi ina manufaa kama vile: husaidia wataalamu katika ubunaji wa mfumo unaofaa wa lugha kienzo ya kuelezea hiponimia za misamiati ya lugha mbalimbali ulimwenguni (Jackson, 1996). Husaidia wataalamu kuonyesha mlinganisho usiowezekana na unaowezekana wa seti za leksimu za lugha husika hasa katika leksikografia linganifu. Hivyo basi hutumiwa kuonyesha ruwaza za miundo ya leksimu za lugha na pia kutafsiri leksimu (Nida, 1975). Hutumiwa kulinganisha visawe kileksikolojia ili kuonyesha kufanana au kutofautiana kwake kimatumizi, kimuktadha na kifahiwa (Bright, 1992; Mathews, 1997). Kwa mfano, ikiwa leksimu ya lugha asilia ina sifa [+a, +b, +c, +d] na kisawe chake katika lugha pokezi kina sifa [+a, +b, +c, -d] basi leksimu hizo zinatofautiana katika sifa bainifu [-d].

Ingawa leksimu hizi zinatofautiana kwa sifa [-d], zinakubaliwa kuwa visawe kwa sababu ya zile sifa zinazofanana za [+a, +b, +c]. Hivyo basi, huweza kutumiwa na wafasiri kutafsiri leksimu ili kuonyesha visawe kamilifu na karibia kwa kutumia alama za [+, -]. Visawe kamilifu hufanana kimaana kiisimu na kimuktadha na visawe karibia hutofautuiana kimaana kwa kiwango fulani kimuktadha (Lyons, 1981). Mathalani, *breakfast* lina kisawe kama vile *kiamshakinywa/chamshakinywa/staftahi/kisebeho* katika lugha ya Kiswahili. Hata hivyo, tunapochunguza maana kwa kina tutapata kuwa leksimu hizi mbili si visawe kamilifu bali ni visawe karibia kwa sababu ya tofauti za kitamaduni.

Kwa mujibu wa *Oxford Advanced Learner's Dictionary* (OALD) (Hornby, 2010:172), *breakfast* ni 'mlo wa kwanza wa siku' na *KKS* (2004:154) inafasili *kiamshakinywa* kama 'chakula cha kwanza cha asubuhi baada ya kuamka'. Ingawa fasili hizi zinalandana kwa kuwa mlo wa kwanza, tofauti huonekana katika yaliyomo. Newmark (1988) anaeleza kuwa *breakfast* [huliwa hadi saa tatu unusu asubuhi, hasa na watu wanaokwenda kazini na aghalabu huhusisha vyakula kama vile *chai*, *kahawa*, *chakula cha nafaka* (cereal), *gurungo* (bacon) na *mayai*].

Katika mabara mengine *breakfast* hujumuisha [*chai, kahawa* na *tosti/tosi* (toast), hutumiwa asubuhi hadi saa tatu unusu na watu wanaokwenda kazini] (Newmark, 1988). Katika jamii za Kiafrika, *kiamshakinywa* hujumuisha [*uji, chai* au *kahawa*] zinazoliwa bure au kwa [*kande/pure, mkate, viazi, ndizi*]. Tazama matumizi ya nadharia ya Uchanganuzi Vijenzi kubainisha *breakfast* na *kiamshakinywa* katika jedwali lifuatalo:

**Jedwali 3: Uchanganuzi Vijenzi katika Visawe *Breakfast* na *Kiamshakinywa***

| | *breakfast* | *kimshakinywa* |
|---|---|---|
| hutumiwa saa tatu unusu asubuhi | + | - |
| hutumiwa wakati wowote asubuhi | - | + |
| hutumiwa na watu wanaokwenda kazini asubuhi | + | - |
| hutumiwa wakati wowote | - | + |
| hujumuisha chai, kahawa, nafaka, gurungo na mayai | + | - |
| huweza kuwa uji, chai, kahawa pamoja na kande, mkate, viazi, ndizi n.k | - | + |

Kwa mujibu wa jedwali, *breakfast* ina sifa bainifu: [+saa tatu unusu asubuhi, -wakati wowote asubuhi, +chakula cha wanaokwenda kazini, -watu wote, +mlo wa chai, kahawa, chakula cha nafaka, gurungo na mayai, -huweza kuwa uji, chai, kahawa pamoja na kande, mkate, viazi, ndizi n.k]. *Kiamshakinywa* ina sifa bainifu za [-saa tatu unusu asubuhi, +wakati wowote asubuhi, -cha watu wanaokwenda kazini, +watu wote, -mlo wa chai, kahawa, chakula cha nafaka, gurungo na mayai, +huweza kuwa uji, chai, kahawa pamoja na kande, mkate, viazi, ndizi n.k]. Hivyo basi, tunapoangazia kisawe katika lugha mbili husika, aghalabu kile kinachoandikwa kama kisawe wakati mwingine huonekana kuwakaribia tu wala si kamilifu. Hii ni kwa sababu ya tofauti kitamaduni na kimuktadha za lugha mbili husika.

## 1.6 Udhaifu wa Nadharia ya Uchanganuzi Vijenzi

Licha ya kwamba nadharia hii ni muhimu katika uchanganuzi wa hiponimia za lugha husika, Mathews (1997) na Ottenheimer (2006) wanaeleza kuwa ina udhaifu kama vile: kwanza, haijulikani iwapo miundo ya hiponimia ni ya kinadharia au ya kisaikolojia na uhusiano wa leksimu kihiponimia haulingani katika lugha zote ulimwenguni. Miundo tofauti tunayopata ni kwa sababu ya athari za ubinafsi wa mtu pamoja na utamaduni wa lugha yake. Kama vile *mnyama kipenzi* (pet), *fanicha/samani, magugu, vifaa* na *uhusiano kijamii* huelekea kuwa tofauti kijamii, kimaeneo na kitamaduni. Pili, Nadharia ya Uchanganuzi Vijenzi haiwezi

kutumiwa katika uchanganuzi wa fahiwa zote kama vile antonimia, homonimia, polisemia na kadhalika na fomyula zake zinaelekea zikibadilikabadilika kila mara kwa mujibu wa ujuzi na uteuzi wa mtafiti (Nida, 1975). Mabadiliko kama haya ya fomyula huonekana tunapoangazia kategoria ya leksimu mbalimbali. Tatu, sifa bainifu za hiponimu hazina maelezo mamoja maalumu na hata alama nyingi hivyo basi watumiaji wake huelekea kueleza sifa za hiponimu kwa kutumia lugha tena. Nne, Nadharia ya Uchanganuzi Vijenzi haitoi nafasi ya kuonyesha mfano bora wa hipanimu husika katika lugha jambo ambalo ni muhimu katika uainishaji wa leksimu kikategoria (Krifka, 2001).

Kwa ujumla, Nida (1975) anaeeleza kuwa udhaifu wa nadharia hii huweza kutazamwa kwa muhtasari kama vile: haina mfumo bia msingi wa lugha kienzo, leksimu zinazotangamana kimaana hutatanisha, hiponimu hutofautiana kiviwango na watafiti wanatofautiana kuhusu sifa bainifu ambazo huwa dhahania. Homonimia na polisemia haziwezi kuchambuliwa kwa kutumia nadharia hii, kuna shida za maana katika leksimu viashiria na mahusiano ya kijamii ni vigumu kubainisha. Vilevile hiponimia huwa changamano katika mahusiano ya maneno ya kuonyesha masharti kama vile iwapo na ingawa. Inadhihirisha ugumu tunapoeleza vijenzi vya hiponimia za leksimu nomino dhahania, vivumishi, vielezi na vitenzi. Hata hivyo, udhaifu wa nadharia ya Uchanganuzi Vijenzi hauwezi kuepukika kwa sababu ya tofauti za lugha kitamaduni na kimazingira (Nida, 1975) na pia ubinafsi wa mtafiti. Tofauti hizi huzua changamaoto ya kupatikana kwa fomyula moja maalumu ya kutumiwa.

Licha ya udhaifu huo, nadharia hii ingali maarufu na aghalabu hufaulu tunapokusanya data kwa kutumia mtindo au modeli tambuzi ya hiponimia kisintaksia katika kongoo maalumu kama ilivyodokezwa na Hearst (1992) na Snow, Jurafsky na Ng (2004). Mtindo huu unaonyesha namna ya kutambua hipanimu na hiponimu katika sentensi kwa kutumia modeli ya [$L_o$ ni aina ya $L_1$] (Hearst, 1992) ambapo ($L_o$) ni hiponimu na ($L_1$) ni hipanimu. Hivyo basi, tunaweza kuwa na [$L_o$ (*gozi*) ni aina ya $L_1$ (*mchezo*)]. Tazama utambuzi wa hipanimu (*mchezo*) na hiponimu (*gozi*) katika dondoo lifuatalo:

[**gozi** *nm* mchezo wa mpira; soka, kabumbu, kandanda] (TUKI, 2004: 100).
|　　　|
hiponimu hipanimu

**1.7 Kufaa kwa Uchanganuzi Vijenzi dhidi ya Nadharia nyingine**

Kuna nadharia nyingi zinazoweza kutumika katika uchanganuzi wa hiponimia. Hata hivyo, hakuna zile zinazoweza kutumiwa bila kuwepo na dosari. Ingawa nadharia ya Uchanganuzi Vijenzi ina udhaifu, kwa upande mwingine inafaa katika

uchanganuzi wa hiponimia ikilinganisha na nadharia nyingine kwa sababu ya mtindo wa kisayansi unaodhihirisha matumizi ya alama za [+, -] na majedwali ya kimatriki yanayoonyesha uwazi wa seti ya sifa bainifu. Nadharia hii inafaa katika uimarishaji wa msingi imara wa matumizi ya nadharia tafsiri ili kuonyesha namna tunavyoweza kupata visawe kamilifu na karibia (Bright, 1992; Mathews, 1997). Visawe hivi ni muhimu katika leksikografia thaniya. Licha ya kutumia alama za [+, -] ili kuonyesha sifa bainifu za hiponimu husika, inahusisha vilevile modeli maalumu inayosaidia katika upataji wa mfumo elekezi wa kutambua haraka hipanimu na hiponimu kwa kuzingatia jinsi zilivyotumiwa katika makala maalumu ya kileksikografia.

Nadharia ya Uchanganuzi Vijenzi ingali maarufu ikilinganishwa na nadharia nyinginezo kama vile 'Kiini Maana' (Core Meanings Theory) na 'Sampuli Kifani' (Protofype Theory). Nadharia ya 'Kiini Maana' iliibuliwa na Labov katika miaka ya 1973 na 'Sampuli Kifani' na Eleanor Rosch katika miaka ya 1975 (Hatch & Brown, 1995) na akaiendeleza 1978, 1983 (Storms, Boeck & Ruts, 2000). Nadharia hizi mbili zinaelekea kuangazia mfano bora wa leksimu tofauti na jinsi nadharia ya Uchanganuzi Vijenzi inavyotumia fomyula kama vile ya kuwa na seti ya sifa maalum (Yule, 1996).

### 1.8 Nadharia ya Kiini Maana

Nadharia ya 'Kiini Maana' inahusisha maana ya neno maalum linalodhukuriwa kama kiini, halisi, la msingi na kujumuisha maneno mengine mahususi (Hatch na Brown, 1995). Kiini ni maana kamilifu, msingi na inayorejelea kirejelewa hata kama umbo lake limeparanganywa. Mathalani, katika jamii ya Wamarekani, kiini maana cha *kikombe* (cup) huelezwa kama [chombo chenye mpini, takriban inchi tatu kwa urefu na pande zake zenye mpindo, hutengenezwa kwa udongo na hutumiwa kunywea kahawa] (Hatch & Brown, 1995). Ili kuainisha leksimu nyingine katika hipanimu *kikombe* basi lazima mtafiti ajaribu kuangazia vile vyombo vyenye umbo na kiini maana kama inavyoelezwa kuhusu *kikombe* asilia cha Kimarekani. Inabainika kuwa Nadharia ya Kiini Maana haina fomyula tegemezi maalum ya kutumiwa katika uchanganuzi wa hiponimia. Hivyo basi, nadharia hii huweza kumfanya mtaalamu kufikiria tu kuhusu neno la kimsingi pasipokutilia maanani vigezo msingi vya kuhusisha maana za maneno mengine ndani yake. Hii ni kwa sababu iwapo kuna *kikombe* kisicho na mpini wala urefu wa inchi tatu basi bado kitaitwa *kikombe* au ni kitu kingine tofauti.

Tunaweza kuangazia mfano wa matumizi ya Nadharia ya Kiini Maana kwa kurejelea leksimu *mlango*. Aghalabu *mlango* huwa na kiini maana kuwa 'kizuizi kilichotengenezwa kwa ubao, chuma au kitu kingine chochote kwenye ukuta au kiambaza cha jengo, chumba au gari' (TUKI, 2004:259). Kiini maana

kinachoonekana katika *mlango* ni kwamba aghalabu hupatikana ukutani au kiambazani. Hata hivyo, huenda tutachanganyikiwa kutokana na maelezo kama hayo iwapo pana chombo kingine chenye jukumu kama la mlango kwenye paa la nyumba au sakafu. Je, bado chombo hicho kitaitwa *mlango* au ni kitu kingine tofauti?


## 1.9 Nadharia ya Sampuli Kifani

Nadharia ya Sampuli Kifani iliasisiwa na Eleanor Rosch katika miaka ya 1975 na kuiendeleza katika miaka ya 1978 na 1983 (Storms, Boeck & Ruts, 2000). Nadharia hii hurejelea hali ambapo hiponimu kadha zinakuwa mfano bora au kufaa kwa dhana au hipanimu maalumu (Hatch & Brown, 1995). Inaeleza kuwa kuna orodha au seti ya sifa za kitu ambazo zinakifanya kudhukuriwa kama mfano bora wa hipanimu maalum na sifa hizo huwa za viwango mbalimbali (Storms na wenzie 2000; Kittur, Holyoak na Hummel, 2006). Kama vile *kurumbiza* (robin) ni mfano wa kiwango bora cha *ndege* (bird), *mwailoni* (oak) ni mfano bora wa *mti* (tree) (Hatch na Brown, 1995). Japo, *njiwa* (dove), *bata* (duck), *flamingo*, *kasuku* (parrot), *mwari* (pelican) na *kijumbamshale/mbayuwayu* (swallow) ni hiponimu za *ndege* (bird), hazidhukuriwi kama mfano bora wa *ndege* (Yule, 1996).

Watumiaji wengi wa Kiingereza huelekea kudhukuru *kurumbiza* kama mfano bora wa *ndege* kwa sababu huwa na sifa msingi za [+mbawa, +manyoya, +hupaa, +mdomo uliochongoka, +hutaga na kuangua mayai]. Hivyo basi, *mbuni* (ostrich) na *pengwini* (penguin) huenda hawatachukuliwa mara moja kama mfano bora wa *ndege* kwa sababu ya kutoafikiana na baadhi ya sifa hizo bia kama vile [-hupaa]. Hata hivyo, *shorewanda* (sparrow) na *njiwa* (pigeon) ni mifano iliyo karibu mno na *ndege* kuliko *mbuni* na *pengwini*. Vilevile watu huelekea hutambua haraka *kiti* (chair) kama mfano bora wa *fanicha/samani* (furniture) kuliko *benchi* (bench) na *stuli/kigoda* (Yule, 1996).

Kwa kiwango fulani Nadharia ya Sampuli Kifani inaelekea kuchanganya matumizi ya sifa bainifu na kipimo cha viwango vya mfano bora ili kugundua hiponimu za hipanimu husika. Mathalani, tukitumia Nadharia ya Sampuli Kifani katika orodha hii ya leksimu [*mnyama, kuku, ndege* na *kurumbiza*], basi tutakuwa na hipanimu *mnyama* inayojumuisha *ndege*. Mfano bora wa *ndege* utakuwa kama vile *kurumbiza* kisha hufuatwa na *kuku* mtawalia. Utaratibu huu huonyesha moja kwa moja kuwa leksimu iliyo na sifa zinazofanana na hipanimu hurejelewa kama mfano bora wa kiwango cha juu na kufuatana hadi hiponimu ya mwisho (Krifka, 2001). Tazama maelezo hayo katika kielelezo kinachofuatia:

**Kielelezo 1: Sifa za Leksimu kwa mujibu wa Nadharia ya Sampuli Kifani**




Kwa mujibu wa kielelezo hiki, *ndege* ipo karibu na *mnyama* kuliko *kurumbiza* na *kuku*. Tunapochukua *ndege* kama hipanimu, basi *kurumbiza* yenye sifa [$S_1$ $S_2$ $S_3$] hudhukuriwa kama mfano bora kuliko *kuku* yenye sifa [$S_1$ $S_2$ $S_3$ $S_4$]. Tofauti baina ya *kurumbiza* na *kuku* ni kuwepo kwa sifa bainifu [$S_4$] ya *kuku.* Kutokana na sifa hii ya [$S_4$], tofauti za maana za *kurumbizi* na *kuku* huonekana vilevile hata katika *KKS* kama vile:

**Kuku** *nm* ndege anayefugwa na anayefanana sana na kware mkubwa (TUKI, 2004: 198).

**Kurumbiza** *nm* ndege mdogo mwenye kichwa cheusi, mgongo na mbawa za kahawia, rangi iliyoiva kifuani na tumboni (TUKI, 2004:201).


*Kurumbiza* na *kuku* zina sifa inayolandana kama vile [+ndege]. Hata hivyo zinatofautina kwa kuwa *kuku* ina sifa [+anayefugwa] huku *kurumbiza* ikiwa na sifa [-anayefugwa]. Sifa inayotozifautisha ni [$S_4$] yaani [+anayefugwa].

Nadharia ya Sampuli Kifani husaidia katika uainishaji wa hiponimia kwa kurejelea sifa za ukubwa na mkao wa umbo la kirejelewa (Hatch na Brown, 1995). Pia, ni muhimu katika uwekaji kikategoria wa mifano bora ya hipanimu, husaidia watoto kung'amua haraka mifano bora miongoni mwa misururu ya hiponimu husika na hutumiwa kama jukwaa la utambuzi wa kirejelewa (Hatch na Brown, 1995). Ingawa ni nadharia muhimu, ina shida kuwa kile kinachodhukuriwa kama mfano bora kwa mtu mmoja huenda ni tofauti na mfano bora kwa mwingine kutokana na utamaduni wao. Kwa mfano, sampuli kifani za *kitoweo* huweza kuwa [*samaki, kuku* na *nyama ya ng'ombe*] hata hivyo wengine huweza kutaja [*nyama ya mbwa* na *nyama ya paka*]. Nadharia hii huelekea kutatanisha hiponimia ya leksimu vielezi, vivumishi na vitenzi. Mathalani, *vuli, masika* na *kipupwe* zinarejelewa kama hiponimu za *majira* hata hivyo tutashindwa kutaja ni upi mfano bora? Kwa ujumla, Asher (1994) anaeleza kuwa: uainishaji wa mfano bora wa dhana au hipanimu hauwezi kuwa na fomyula moja. Kila mtu binafsi anaweza kujitokeza na fomyula yake anaposhughulikia hiponimia hivyo basi haiwezi kutumiwa kuchanganua dhana zote kama zile changamano (Kamp na Partee, 1995). Vilevile maana za virejelewa vya mfano bora wa hipanimu huelekea kuzunguka na

kujengwa kutokana na maana ya hipanimu hiyo hiyo (Asher, 1994). Aidha, inadhihirika kuwa hiponimu wanachama wa hipanimu huelekea kushirikiana kwa viwango tofauti tofauti huku mifano mingine iliyo mbali na maana msingi ya dhana husika huelekea kutoelezwa vizuri. Si kila mfano bora wa hipanimu huwa bora moja kwa moja kwa sababu kuna mifano mingine iliyo bora kushinda mingine na pia huathiriwa na utamaduni wa watu.

Viwango vya uainishaji wa hiponimu hutegemea kipimo cha viwango kinachojulikana kama 'Goodness-of-Exemplar Ratings' (GOE ratings) chenye viwango [1-7] vilivyopendekezwa na Rosch (Cruse, 2011: 57). Kila kiwango huwa na alama yake kama vile: [1] Mfano bora zaidi (Very good example), [2] Mfano bora (Good example), [3] Bora ya kuridhisha (Fairly good example), [4] Bora kiasi (moderately good example), [5] Mfano mbaya kiasi (Fairly bad example), [6] Mfano mbaya (Bad example) na [7] Mfano mbaya zaidi/si mfano kabisa (very bad example/not example at all). Tafiti nyingi zimedhihirisha kuwa usampuli kifani unashabihiana moja kwa moja na kipimo cha viwango vya mfano bora wa hipanimu (Kittur, Holyoak na Hummel, 2006). Watafiti wengi wanawasilisha sampuli kifani kwa tumia mduara (Aitchison, 1987: 54 katika Hatch na Brown (1995: 54) kuhusu hiponimu za *ndege*:

**Kielelezo 2: Kielelezo Mduara cha Hiponimu za *Ndege***



Kwa mujibu wa kielelezo hiki, mfano bora zaidi wa hipanimu *ndege* hufuatana kiviwango kutokea [*kurumbiza*], [*njiwa* na *shorewanda*], [*bundi, kwale* na *kasuku*], [*tausi* na *bata*] na hatimaye [*pengwini* na *mbuni*] zinazoelekea kuchukua nafasi ya mwisho kwani ni mifano lakini si mifano bora zaidi. Hata hivyo, viwango hivi huonekana kana kwamba si asilia, hutegemea muktadha, mpaka wa kategoria hauonekani na mifano inayotolewa huweza kujitokeza kuwili kiuamilifu (Cruse, 2011).

## 1.10 Hitimisho

Nadharia ya Uchanganuzi Vijenzi imeelezwa kama ile nadharia inayochanganua sifa bainifu za hiponimu zinazojumuishwa katika uwanda mmoja kileksika na kisemantiki kwa kutumia alama za [+, -] zinazotumiwa kuonyesha ama kuwepo au kutokuwepo kwa sifa husika. Chimbuko la Nadharia ya Uchanganuzi Vijenzi ni nadharia ya Uwanda Kisemantiki na Uwanda Kileksika na maendeleo yake yanaweza kuangaziwa kutokana na mfumo wa sifa za kifonetiki za fonimu za lugha kama ulivyozingatiwa na wanaskuli wa Prague. Nadharia ya Uchanganuzi Vijenzi inaonyesha ufafanuzi wa mielekeo ya sifa za leksimu katika hiponimia kiisimu na pia kisayansi. Nadharia hii inahusisha taratibu zake kama vile kutambua au kuteua hiponimu na hipanimu katika kongoo, kuorodhesha hiponimu kialfabeti, kubainisha sifa za hiponimu kwa kutumia alama za [+, -], kuonyesha sifa zinazolingana na zisizolingana miongoni mwa hiponimu husika, kupitia tena data husika na hatimaye kufasili sifa husika katika vielelezo na majedwali.

Nadharia hii ina natija kama vile husaidia katika ubunaji wa mfumo faafu wa lugha kienzo ya kuelezea hiponimia ya misamiati mingi ya lugha mbalimbali ulimwenguni, huonyesha mlinganisho usiowezekana na unaowezekana wa seti za leksimu za lugha husika hasa katika leksikografia linganifu na pia hutumiwa katika kutafsiri leksimu. Nadharia ya Uchanganuzi Vijenzi inaweza kutumiwa kulinganisha kileksikolojia leksimu za lugha moja hasa visawe ili kuonyesha kufanana au kutofautiana kwake kimatumizi, kimuktadha na kifahiwa.

Hata hivyo, nadharia hii ina udhaifu wake kwamba haijulikani iwapo hali ya miundo ya hiponimia ni ya kinadharia au ya kisaikolojia na pia uhusiano wa leksimu kihiponimia haulingani katika lugha zote ulimwenguni na haiwezi kutumiwa katika uchanganuzi wa fahiwa zote za leksimu za lugha kama vile antonimia, homonimia, polisemia na kadhalika. Pia, fomyula zake zinaelekea zikibadilikabadilika kila mara kwa mujibu wa ujuzi na uteuzi wa mtafiti husika, sifa bainifu za leksimu husika yaani hiponimu hazina maelezo maalum na alama hivyo basi huelekea kuelezwa tena kwa kutumia lugha. Nadharia ya Uchanganuzi

Vijenzi haitoi nafasi ya kuonyesha mfano bora wa hipanimu husika katika lugha jambo ambalo ni muhimu katika uainishaji wa leksimu kikategoria au kihiponimia.

Licha ya kuwa nadharia ya Uchanganuzi Vijenzi ina udhaifu, kwa upande mwingine ina manufaa makubwa inapolinganishwa na nadharia nyingine kama vile nadharia ya Kiini Maana (Core Meanings Theory) inayochunguza maana msingi ya hipanimu na hatimaye kujumuisha hiponimu zake na nadharia ya Sampuli Kifani (Prototype theory) inayoangazia suala la kuwepo kwa hiponimu inayodhukuriwa kama mfano bora wa hipanimu husika. Nadharia hizi mbili zinaelekea kutawaliwa na ubinafsi mwingi wa mtafiti na utamaduni wa lugha bila kuwa na fomyula yoyote ya ama kiisimu au kisayansi na pia ukubwa na umbo la viashiria husika.

## Marejeo


Aitchison, J. (2003). *Linguistics*. London: Hodder & Stoughton, Ltd.

Asher, R. E. (Mh) (1994). *The Encyclopedia of Language and Linguistics*. Vol. 6. Oxford: Pergamon Press.

Bright, W. (1992). *International Encyclopedia of Linguistics.* Vol. 1 & 2. Oxford: Oxford University Press.

Bussmann, H. (1996). *Routledge Dictionary of Language and Linguistics*. London: Rout ledge.

Cable, S. (2009). Some Basic Facts about the Dholuo Language. Katika: *Structure of a Non-Indo-European Language Fall 2009 Ling748*, uk 1-13. Kupatikana Novemba 25, 2011 kutoka people.umass.edu/scable/LING748-FA09/Materials/Handouts/Dholuo-Basics.pdf

Crystal, D. (1987). *Child Language Learning and Linguistics: An Overview for the Teaching and Therapeutic Professions.* London: Edward Arnold.

________. (1992). *An Encyclopedic Dictionary of Language and Linguistics.* UK: Blackwell.

Fromkin, V., Rodman, R., & Hyams, N. (2007). *An Introduction to Language*. Boston: Thomson Wadsworth.

Goodenough, W. H. (1956) Componential Analysis and the Study of Meaning. Katika**:** *Language*, Vol. 32, No. 1. (Jan. - Mar., 1956), uk 195-216. Imepakuliwa Machi 15, 2012 kutoka http://www.anthro.ucsd.edu/~jhaviland/LanguageCulture/READINGS/Goodenough/KinshipLanguage.1956.pdf

Hatch, E., & Brown, C. (1995). *Vocabulary, Semantics and Language Education.* Cambridge: Cambridge University Press.

Hearst, M. A. (1992). Automatic Acquisition of Hyponyms from Large Text Corpora. Proceedings of Coling-92, Agosti 23-28, uk 539-545. Berkely: University of California Computer Science Division & Xerox Palo Alto Research Center. Kupatikana Desemba 6, 2011 kutoka http://delivery.acm.org/10.1145/1000000/992154/P539hearst.pdf?Ip=197.156.120.168acc=OPEN&CFID=56549492&CFTOKEN=65441157&_acm_=132316

Hjelmslev, L. (1970). *Language: An Introduction*. Madison: The University of Wisconsin Press.

Hornby, A. S. (Mh.) (2010). *Oxford Advanced Learner's Dictionary*. 8th Ed. Oxford: Oxford University Press.

Jackson, H. (1996). *Words and Their Meanings*. New York: Addison Wesley Longman Inc.

Jensen, K. E. (2008). *Translation and Translation Theory*. Lecture notes, Week 1(36). University of Alborg.

Kamp, H., & Partee, B. (1995). Prototype Theory and Compositionality. Katika: *Cognition 57*, uk129-191. Kupatikana Machi 15, 2012 kutoka http://semantics.uchicago.edu/kennedy/classes/s06/readings/Kamp-Partee95.pdf

Katz, J. (2004). *Sense, Reference and Philosophy*. Oxford: Oxford University Press.

Katz, J. J., & Fodor, J. A. (1963). The Structure of the Semantic Theory. Katika Jakobovits, M. M. *Readings in the Psychology of Language*. Englewood Cliffs: Prentice Hall.

________. (1981). *Language and Other Abstract Objects*. Totowa: N. J. Rowman and Littlefield.

Koulikova, R. (2006). A Contrastive Componetial Analysis of Motion Verbs in English and Swedish. Katika: *Linguistics in the Midnight Sun, Report No.6*. Lulea University of Technology: Department of Languages and Culture. Kupatikana Juni 13, 2012 kutoka http://epubl.ltu.se/1402-1773/2006/050/LTU-CUPP-)6050-SE.pdf

Kreidler, C. (2002). *Introducing English Semantics.* New York: Routledge.

Krifka, M. (2001). *Semantic Fields and Componential Analysis*. Humboldt Universitat zu Berlin: Institut fur deustsche prache und Linguistik. Kupatikana Machi 15, 2012 kutoka http://amor.cms.huberlin.de/~h2816i3x/Lehre/2001_Hs_Lexika/ischesemantik/lexSemantik2.pdf

Leech, G. (1976). *Semantics.* Harmondsworth: Penguin Ltd.

Lehrer, A. (1974). *Semantic Fields and Lexical Structure*. Amsterdam: North Holland.

Lipka, L. (1986). Semantic Features and Prototype Theory in English Lexicology. Katika: D. Kastovsky, & A. Szwedeck (Wh.) *Linguistics across Historical and Geographical Boundaries*, Vol. 1. uk 85-94, Berlin; New York; Amsterdam: Mouton de Gruyter. Kupatikana Machi 15, 2012 kutoka http://epub.ub.uni-muenchen.de/5095/1/5095.pdf

Longhorn (2011). *Kamusi ya Karne ya 21*. Nairobi: Longhorn.

Lounsbury, F. G. (1963). The structural analysis of kinship semantics. In H. Lunt (Mh.). *Proceedings of the ninth international congress of linguists* 1073-93. The Hague: Mouton.

Mathews, P. H. (1997). *The Concise Oxford Dictionary of Linguistics*. Oxford: Oxford University Press.

Mgullu, R. S. (1999). *Mtalaa wa Isimu. Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili*. Nairobi: Longhorn Pulishers.

Miller, A. G. (1991). *The Science of Words*. New York: Scientific American Library.

Munyua, J. G. (1999). Kanuni za Uteuzi zuifu na Uhuru wa Msanii: Mifano katika Kiswahili. Makala iliyowasilishwa katika semina ya Idara, Mei 17-18. Chuo Kikuu cha Moi: Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika.

Newmark, P. (1988). *A Text book of Translation*. New York: Prentice Hall International.

Nida, E. A. (1975). *Componential Analysis of Meaning*. Belgium: Mouton Ottenheimer, H. J. (2006). *The Anthropology of Language.* Belmet, C. A.: Thomson Wadsworth.

Prinsloo, D., Chuwa, A. R., & Taljard, E. (2000). The Lexicons of Africa. Katika: V. Webb, & Kembo - Sure (Wh.) *African Voices: An Introduction to Language and Linguistics of Africa.* Southern Africa: Oxford University Press, uk 220-44.

Saeed, J. (2009). *Semantics.* 3rd ed. United Kingdom: Wiley Blackwell.

Snow, R., Jurafsky, D., & Ng, A. Y. (2004). *Learning Syntactic Patterns for Automatic Hypernym Discovery*. Stanford: Stanford University. Kupatikana Desemba 06, 2011 kutoka http://www.Stanford.edu/jurafsky/paper 887.pdf

Tucker, A. N. (1994). *A Grammar of Kenya Luo (Dholuo).* Koln: Rudiger Koppe Verlag

TUKI (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi: Oxford University Press.

Wardhaugh, R. (1977). *Introduction to Linguistics*. United States: McGraw-Hill.

Yule, G. (1996). *The Study of Language*. 2nd ed. Cambridge: Cambridge University Press.